

Tathmini ya Mikakati ya Tafsiri ya Vinay na Derbelnet (2004) katika Tafsiri ya A Good Day (2019)

Sarah Ndanu M. Ngesu¹, Pendo Salu Malangwa² na Mosol Kandagor³

¹*Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya*

²*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

³*Chuo Kikuu cha Moi*

Ikisiri

Uteuzi wa mikakati ya tafsiri katika mchakato wa tafsiri, ni suala muhimu katika Nadharia ya Tafsiri. Lengo la makala haya ni kutathmini mikakati ya tafsiri iliyotumiwa katika kutafsiri ya riwaya ya Kiswahili *Siku Njema* iliyotafsiriwa kwenda Kiingereza kama *A Good Day*. Uteuzi wa mikakati ya tafsiri unaweza kuwa na athari zake katika uhawilishaji wa ujumbe. Hata hivyo, suala hili halijapewa nafasi inayostahiki katika tafiti tangulizi kuhusu kazi za tafsiri. Tathmini za tafsiri hujikita kuchanganua changamoto za tafsiri bila kuonesha kwamba uteuzi wa mikakati ya tafsiri una mchangano mkubwa katika kuibua changamoto hizo. Modeli ya Vinay na Derbelnet (2004) ilitumiwa kubaini mikakati ya tafsiri iliyotumiwa na wafasiri Dorothy Kweyu na Fortunatus Kawegere. Wataalamu wanakubaliana kwamba Modeli ya Vinay na Derbelnet ndio msingi wa uainishaji wa mikakati ya tafsiri na wataalamu wengine wanaoainisha mikakati ya tafsiri hutumia modeli hii kama msingi wa uainishaji wao.

Maneno Muhimu: Mikakati ya Tafsiri, *Siku Njema*, *A Good Day*

Utangulizi

Ijapokuwa tafsiri huonekana kama mchakato wa kuhamisha ujumbe kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa, kulingana na Nida na Taber (1969), tafsiri ni mchakato unaohusisha mambo mengi. Mihimili mikuu ya tafsiri ni kufanya uchanganuzi, kuhawilisha na kuandika upya ujumbe kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Katika hatua ya uchanganuzi, mfasiri huchunguza kwa makini muundo wa ujumbe wa lugha chanzi, maana ya maneno, vishazi na sentensi ili kumwezesha kuelewa ujumbe mzima. Hatua ya pili ni kuhawilisha ujumbe kama alivyouelewa kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Hatua ya tatu na ya mwisho ni kuhakikisha uhawilishaji wa ujumbe umekitwa katika muktadha wa hadhira lengwa. Kulingana na Larson (1984), vipengele muhimu katika mchakato

wa tafsiri ni kutalii na kuchanganua maneno, muundo wa kisarufi, na muktadha wa kiutamaduni ili kuelewa ujumbe uliomo katika matini chanzi. Baada ya hatua hiyo ndipo mfasiri huweza kuhawilisha ujumbe katika lugha lengwa kwa kutumia maneno na muundo wa lugha lengwa. Mchakato huu huhusisha uteuzi wa mikakati ya tafsiri inayomsaidia kutatua tatizo la kutafsiri vipashio vikubwa na vidogo vya lugha chanzi.

Wataalamu mbalimbali wametoa fasili anuwai kuhusu mikakati ya tafsiri. Hata hivyo, hatukuweza kuzifafanua fasili hizo zote, bali baadhi ya wataalamu, yaani Bell na Candlin (1991), Nord (1997), Chesterman (1997), Vinay na Derbelnet (2004), Yang Yang (2010) na Azar (2018) wamebainishwa na fasili zao kufafanuliwa.

Bell na Candlin (1991) wanaeleza tofauti kati ya mikakati ya jumla na mikakati bainifu. Kulingana na wataalamu hawa, mikakati ya jumla inajitekeza katika kiwango cha jumla (makro) au upana wa matumizi ya mikakati (Yang Yang, 2010). Mikakati ya jumla huathiri matini nzima ambapo mikakati bainifu huathiri vipashio vya matini inayotafsiriwa. Muktadha wa mikakati ya jumla na mikakati bainifu huelezwa na wataalamu kwa kutumia istilahi tofauti. Nord (1997) anaeleza kwamba mikakati ya tafsiri inaweza kuegemea utamaduni wa lugha chanzi au utamaduni wa lugha lengwa. Chesterman (1997) anaeleza kwamba ni muhimu kutambua aina mbili za mikakati ya tafsiri, yaani mikakati ya jumla na mikakati bainifu. Kulingana na Chesterman, mikakati ya tafsiri ya jumla hutumika kwa ujumla huku mikakati bainifu ikitumiwa katika vipengele maalumu. Maoni haya yanaungwa mkono na Jaaskelainen () anaposema kwamba mikakati bainifu huwa ni taratibu maalum zinazohusishwa na vipengele vya kileksika. Akishadidia maoni haya David Bergen kama anavyonukuliwa na Yang Yang (2010:29) anasema:

If meta-strategies such as those described by Lorscher are the skeleton of translation competence and global strategies as those explained in the previous section are the muscles, local strategies could be compared to many vital systems which deliver air, nourishment, blood and hormones to the various parts of the body to keep functioning well.

Ikiwa mikakati moja kwa moja kama inayofafanuliwa na Lorscher ndiyo muundo wa mifupa ya umilisi wa tafsiri na mikakati ya jumla iliyoelezwa katika sehemu ya awali ni misuli, mikakati ya moja kwa moja inaweza kulinganishwa na viungo muhimu vinavyosambaza hewa, chakula, damu na homoni katika sehemu mbalimbali za mwili ili kuhakikisha unaendelea kufanya kazi vyema (Tafsiri ni yetu).

Akishadidia hoja kwamba kuna tofauti baina ya mikakati ya tafsiri na mbinu za tafsiri, Molina na Albir (2002: 507) wanasema:

Translation method refers to the way a particular translation process is carried out in terms of the translator's objective, i.e, a global action that affects the whole text.

Mbinu ya tafsiri inahusu namna mchakato wa tafsiri unavyoendeshwa kulingana na lengo la mfasiri yaani kitendo cha jumla kinachoathiri matini nzima (Tafsiri yetu).

Maelezo haya yanaonesha kwamba mbinu za tafsiri hutumiwa katika kushughulikia matini yote. Kwa mfano, mfasiri anaweza kuamua kuchukua mwelekeo wa kimawasiliano badala ya tafsiri sisisi katika kutafsiri matini fulani. Molina na Albir (2002) wanatoa mifano ya mbinu za tafsiri zifuatazo: ufasiri wa kimawasiliano, tafsiri sisisi, tafsiri huru na tafsiri ya kifilolojia (kiakademia na tafsiri ya kiuhakiki). Kuhusu mikakati, Molina na Albir (2002) wanaeleza kwamba mikakati ni taratibu (kwa kujua au kutojua, ya kusemwa au ya ishara) inayotumiwa na mfasiri kutatua matatizo yanayotokea anaposhughulika na mchakato wa tafsiri akiwa na lengo mahususi. Waandishi wa makala haya wanakubaliana na maoni ya wataalamu hawa kwamba baada ya mfasiri kuamua mwelekeo wa kutafsiri matini nzima kama vile wa kimawasiliano, huru, wa sisisi au wa kifilolojia, huchukua hatua nyingine ya kutumia mikakati ya tafsiri kukabiliana na matatizo ya kutafsiri. Mikakati hii huitumia kutafsiri vipashio vidogo ndani ya matini hiyo.

Kuna mengi yaliyoandikwa kuhusu mikakati ya tafsiri katika mchakato wa kutafsiri matini na pia kuhusu mbinu ya tafsiri katika ufundishaji wa lugha ya kigeni. Hata hivyo, utafiti huu umebaini kwamba kuna maandiko machache yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili kuhusu mikakati ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Kwa mujibu wa Pjuastuti (2014), mikakati ya tafsiri ni njia au taratibu anazotumia mfasiri katika kutafsiri maneno, vishazi na sentensi kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Newmark (2003) anatumia jina la taratibu za tafsiri. Anaeleza kwamba taratibu za tafsiri ni mchakato wa kuhamisha sentensi na vipashio vingine vidogo kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa.

Vinay na Derbelnet wanaeleza kwamba msingi wa uteuzi wa mikakati ya tafsiri ambayo mfasiri anaweza kuteua ni mikakati miwili. Waliainisha mikakati ya tafsiri katika makundi mawili: tafsiri ya moja kwa moja na tafsiri isiyo wazi. Kuhusu mikakati ya moja kwa moja, Vinay na Darbelnet wanaeleza kwamba huu ni uteuzi wa kategoria za kisarufi au visawe vya dhana vinavyolingana baina ya lugha chanzi na lugha lengwa. Kuhusu tafsiri isiyo wazi wanasema, kwamba inahusu uteuzi wa mikakati inayoweza kukabiliana na changamoto za tafsiri ya vipengele visivyokuwa na visawe vya moja kwa moja. Kulingana na Dai (2015), hali hii hutokana na tofauti za kumuundo, kimitindo na kiutamaduni baina lugha

chanzi (kuanzia sasa, LC na lugha lengwa (kuanzia sasa, L L kama anavyoolewa Dai, 2015).

Vinay na Darbelnet (2004) wanatoa mifano ya tafsiri ya moja kwa moja kama vile: ukopaji, tafsiri ya dhana na tafsiri sisisi. Kuhusu mikakati ya jumla/isiyo ya wazi, wanatoa mifano minne: uhamishaji, usawe, ubadilishaji na urekebishaji. Kwa mfano, vipashio vya lugha chanzi vinaweza kuwa na visawe katika lugha lengwa. Katika hali hii lugha chanzi na lugha lengwa huwa na ulinganifu wa kumuundo. Pia, dhana za lugha chanzi zinaweza kuwa na visawe katika lugha lengwa (ulinganifu wa dhana). Hata hivyo, mfasiri anaweza kukabiliana na changamoto za kutokuwepo na ulinganifu wowote baina ya dhana katika lugha chanzi na lugha lengwa. Hata hivyo ni muhimu kueleza kwamba lazima ujumbe wa lugha chanzi uhawilishwe kwenda lugha lengwa. Jukumu la mfasiri ni kuteua mikakati mwafaka itakayofanikisha uhawilishaji wa ujumbe.

Halikadhalika, kama wanavyokubaliana Reza (2018), Dyachkoas (2018) na Pendit (2019), mfasiri anaweza kukabiliana na miundo tofauti ya lugha chanzi na lugha lengwa ambayo haiwezi kuruhusu uhamishaji wa mtindo bila kuvunja sheria za kisintaksia na kileksika za lugha chanzi. Kwa hivyo, mfasiri hulazimika kutumia mikakati ambayo si ya kawaida ili kuweza kukubaliana na changamoto hizo. Mikakati hii hujulikana kama mikakati isiyo ya moja kwa moja. Utafiti wa wataalamu hawa ni muhimu kwa kuwa unaonesha kwamba uteuzi wa mikakati unaweza kuwa na athari zake katika uhawilishaji wa ujumbe. Hata hivyo, uchanganuzi huu ulihusu tafsiri za matini za kimaandishi ambazo vipengele vya kiisimujamii na kimuktadha vinavyoitokeza katika mazungumzo baina ya mwalimu na mwanafunzi darasani havikushughulikiwa.

Vilevile, ni muhimu kueleza kwamba kuna mitazamo tofauti kuhusu matumizi ya mikakati ya tafsiri kama ilivyoelezwa kwenye tatizo la utafiti. Wanazuoni Newmark (2003), Malangwa (2014) na Munday (2016) wanakubaliana kwamba kuna tofauti baina ya mbinu na mikakati. Vilevile, kuna wanazuoni wanaotumia istilahi ‘mikakati’, ‘mbinu’ na ‘taratibu’ kwa maana ya mbinu/mikakati (Lorschester, 1991; Chesterman, 1997; Jilala, 2014). Pia, wapo wanaotambua mbinu pekee na hawazungumzii suala la mikakati, kama vile Mwansoko na wenzake (2015). Kwa mujibu wa Newmark (2003), mbinu za tafsiri huteuliwa kulingana na aina ya matini, walengwa na lengo la tafsiri. Hii ina maana kwamba matini inaweza kuchukua mwelekeo wa tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki au tafsiri ya kimawasiliano. Kuhusu mikakati katika tafsiri, wanazuoni wanaelekea kutofautiana kiistilahi. Kulingana na Munday (2016), mikakati ni jinsi ya kuamua kutumia njia fulani ili kutafsiri vipashio kwenye matini. Hii ina maana kwamba, mbinu hutumiwa katika kutafsiri matini nzima ila mikakati hushughulikia vipashio vya lugha kama vile maneno, virai, vishazi na sentensi katika matini moja. Ordudari (2007) anakubaliana na Newmark (2003) kwamba kuna tofauti baina ya mbinu na mikakati ya tafsiri.

Newmark anafafanua kwamba mbinu hutumiwa kutafsiri matini nzima na mikakati ya tafsiri hutumiwa kutafsiri vipashio vidogovidogo vya lugha kama sentensi, vishazi, virai na maneno.

Newmark (2003) anatumia dhana ya ‘taratibu’ kwa maana ya mikakati na kutoa mifano ifuatayo: utumiaji wa visawe vya kiutamaduni, matumizi ya visawe vya kiuamilifu, ufanuzi, usinonimia, tafsiri za dhana, tafsiri ya kiutohozi, uhamishaji, unukuzi, upunguzaji na upanuzi. Kuhusu mbinu gani na mikakati ipi inayofaa, wanazuoni Newmark (2003) na Mwansokona wenzake(2015) wanakubaliana kuwa tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano ndizo mbinu zinazofanikisha tafsiri za matini nyingi. Wataalamu wengine, yaani Nida na Taber (1969), Munday (2016), Malangwa (2014 na 2017) na Wafula (2017) wanaona kwamba uteuzi wa mikakati hutegemea matini, lengo la tafsiri na hadhira lengwa. Hali hii ya kuwepo kwa mitazamo tofauti kuhusu mikakati inayofaa inazua mkanganyiko wa kinadharia na kiutendaji ambao unahitaji kuchunguzwa. Hii ni kwa sababu mchakato wa kutafsiri darasani huhusisha ufundishaji wa vipengele changamani vya lugha ambavyo vinahitaji uteuzi mwafaka wa mikakati mbalimbali ya tafsiri ili kukabiliana na changamoto za kutafsiri.

Uteuzi wa mikakati ya tafsiri hususan ya jumla kwa mujibu wa kaida za kutafsiri, hufanyika kabla ya kuanza kwa mchakato wa kutafsiri. Mfasiri huamua ni mkakati upi atakaotumia ili kuwasilisha ujumbe kutoka LC kwenda LL. Jambo hili linawezekana katika kutafsiri matini lakini linaweza kuwa na changamoto katika muktadha wa darasani. Hali hii inachochea maswali yafuatayo: mosi, je, ni kweli kwamba mwalimu anaweza kuteua mikakati akayotumia kutafsiri vipashio vya lugha anavyofundisha kabla ya somo? Pili, je, ni mikakati ipi anayotumia kutafsiri maneno, vishazi na sentensi?

Sanjun (2012) anaeleza kwamba dhana *strategy* katika tafsiri hutumiwa pamoja na dhana nyinginezo kama vile ‘*technique*’, ‘*method*’, ‘*tactic*’, na ‘*approach*’ kwa maana ile tu moja au kama sinonimu. Hata hivyo, Sanjun anaeleza kwamba hata kama maana ya maneno haya hufanana kwa kiasi fulani, watafiti hutoa fasili mbalimbali za dhana hizi. Kwa hiyo, kuna mkanganyiko katika matumizi na maelezo ya dhana hizi mionganoni mwa wataalamu.

Sanjun (2012) anaeleza kwamba mkanganyiko uliopo mionganoni mwa wataalamu huenda ukaendelea pasipo kuonesha mpaka kamili uko wapi baina ya dhana hizi. Hata hivyo, Sanjun anakubaliana na wataalamu wengine kwamba msingi wa mikakati ya tafsiri unatokana na mikakati miwili mikuu ambayo ni tafsiri huru na tafsiri sisisi. Tafsiri huru inatumika kutafsiri vipashio vingine zaidi ya neno na tafsiri sisisi hutumika kutafsiri maneno. Kwa maoni ya Sanjun, wataalamu tofauti hutumia dhana au istilahi tofauti kurejea dhana hizo mbili.

Mkabala wa Uchanganuzi

Mkabala uliotumiwa katika makala haya ni wa kitaamuli yaani kimaelezo na kiulinganishi. Waandishi walichambua kiulinganishi matini ya Kiswahili ambayo ni riwaya ya *Siku Njema* na matini ya Kiingereza yaani riwaya ya *A Good Day*. Uteuzi wa *A Good Day* ulichochewa na mambo matatu. Mosi, mwelekeo wa hivi karibuni wa kutafsiri kazi za fasihi kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Hapo awali vitabu vingi vya fasihi vimekuwa vikitafsiriwa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Pili, riwaya ya *A Good Day* ni mionganoni mwa riwaya zilizotafsiriwa hivi karibuni. Riwaya hii imetafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza mwaka wa 2019. Tatuhii, riwaya ya *Siku Njema* ni kazi maarufu sana kwa ukwasi wa lugha na maudhui.

Mikakati ya Tafsiri katika Tafsiri ya *A Good Day*

Mikakati ya tafsiri ni njia, taratibu au mbinu zote zozote anazotumia mfasiri akijua au akiwa hatambui ili kukabiliana na tatizo la kutafsiri kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Vinay na Derbelnet (2004) ni wataalamu wa kwanza waliotumia istilahi ya mikakati katika uainishaji wa mikakati mikuu miwili ya tafsiri. Mikakati hii ni mikakati ya moja kwa moja na mikakati isiyo ya moja kwa moja (*oblique translation*). Mikakati hii miwili kila mmoja unagawika na kuwa na mikakati mingine midogo. Kwa ujumla, tumeamua kutumia modeli ya mikakati ya tafsiri iliyopendekezwa na Vinay na Derbelnet kwa sababu uainishaji wao unaonekana kujumuisha baadhi ya mikakati na hata mbinu zilizopendekezwa na wataalamu wengine ndani ya mikakati yao. Pia, walaalamu wengine waliooinisha mikakati ya tafsiri walitumia msingi uliowekwa na Vinay na Derbelnet (1958). Hivyo, tunatambua mikakati hiyo kuwa ya msingi. Aidha, mikakati ya Vinay na Derbelnet ilioneckana kufaa kuchanganua tafsiri ya vipashio vya lugha katika ufundishaji wa Kiswahili. Utafiti ulibaini kuwa mwalimu hutafsiri mara nyingi vipashio vidogovidogo. Mathalani, maneno, virai na sentensi. Vilevile, uanishaji wa Vinay na Derbelnet umegawanya mikakati katika aina kuu mbili, yaani mikakati ya jumla inayoweza kutumiwa kutafsiri matini nzima na mikakati bainifu inayotumiwa kutafsiri vipashio vidogo.

1. Mkakati Mahususi


Vinay na Derbelnet wanatoa mifano ya mikakati ambayo imo katika mkakati mahususi kama ifuatavyo: mkakati wa ukopaji, mkakati wa tafsiri ya dhana na mkatati wa tafsiri sisisi.

i) **Ukopaji (Vinay na Derbelnet)**

Ukopaji ni mkakati wa tafsiri wa kuhamisha neno au dhana ya lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Kuna aina mbili za ukopaji. Ukopaji wa moja kwa moja wa neno la LC kwenda LL bila kulifanyia marekebisho yoyote. Aina ya pili ya ukopaji inahusu kufanyia neno la LC marekebisho (utohozi) ili liendane na kaida za LL. Kulingana na Vinay na Derbelnet (2004), ukopaji ndio mkakati rahisi

katika tafsiri. Mfasiri anapokabiliana na hali ambayo hakuna kisawe cha lugha chanzi katika lugha lengwa, hukopa neno au dhana ya lugha lengwa aidha vile ilivyo au kwa kulitohoa. Hali ya kutokuwa na usawe baina ya lugha chanzi na lugha lengwa husababishwa na teknolojia ya kisasa inayoingiza maneno na dhana ngeni kwa kasi kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Halikadhalika, vipengele vya kitamaduni na majina ya pekee husababisha ukopaji wa moja kwa moja (kuhamisha neno la LC vile lilivyo kwena LL). Wataalamu Vinay na Derbelnet wanaamini kwamba maneno mengi ya mkopo yalipenyezwa katika lugha kuititia mkakati huu na hatimaye kukubalika kama msamiati wa lugha lengwa. Kielelezo Na. 1 kinaonesha aina hizi mbili za ukopaji.

Kielelezo Na. 1: Aina za Ukopaji



Uchanganuzi wa matini uliojenga msingi wa makala haya unaonesha kwamba aina zote za ukopaji zilitumiwa na wafasiri walioatafsiri Riwaya ya *Siku Njema* kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza (*A Good Day*). Jedwali Na. 1 linaonesha mifano ya ukopaji wa moja kwa moja. Katika hali hii, majina ya watu, mahali na vitu yamehamishwa vile yalivyo kutoka lugha chanzi (Kiswahili) kwenda lugha lengwa (Kiingereza) kama inavyooneshwa hapa chini.

Jedwali Na. 1: Tafsiri ya Moja kwa Moja - Majina ya Watu

| Lugha Chanzi (Kiswahili) | Lugha Lengwa (Kiingereza) | Ukurasa (Matini Tafsiri) |
|---------------------------|---------------------------|--------------------------|
| Zainabu Makame | Zainabu Makame | uk.1 |
| Mzee Mwinyi Makame | Mzee Mwinyi Makame | uk.1 |
| Kitwana | Kitwana | uk.36 |
| Mwana Saumu | Mwana Saumu | uk.37 |
| Vumilia | Vumilia | uk.12 |
| Abdallah | Abdallah | uk.12 |
| Kongowea Mswahili | Kongowea Mswahili | uk.64 |
| Enoch Minja | Enoch Minja | uk.23 |
| Rahma | Rahma | uk.23 |
| Juma Mukosi | Juma Mukosi | uk.32 |
| Kazikwisha | Kazikwisha | uk.124 |
| Athman | Athman | uk.34 |
| Rehema | Rehema | uk.26 |
| Salim | Salim | uk.40 |
| Mzee Mapunda | Mzee Mapunda | uk.43 |
| Mzee Uledi Makali | Mzee Uledi Makali | uk.45 |
| Khamis | Khamis | uk.45 |
| Rashid | Rashid | uk.63 |
| Zawadi | Zawadi | uk.74 |
| Amina | Amina | uk.95 |
| Bakari | Bakari | uk. 66 |
| Selemani | Selemani | uk.21 |
| Mercy Macdonald | Mercy Macdonald | uk. 115 |
| Alice | Alice | uk 113 |
| Nambuye Pilipili | Nambuye Pilipili | uk.119 |
| John Amon | John Amon | uk.122 |
| Butambo | Butambo | uk.96 |
| Daniel | Daniel | uk.96 |

Chanzo: Data Kutokana na Uchambuzi wa Riwaya ya *A Good Day*, 2019

Tungependa kueleza kwamba majina ya watu ni mengi katika riwaya hii. Hata hivyo, hatungeweza kuyaonesha yote ila yote yamehamishwa vile yalivyokuwa katika lugha chanzi. Vilevile, majina ya mahali yalikopwa kutoka lugha chanzi na kuhamishwa kwenda lugha lengwa vile yalivyokuwa kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2 hapa chini.

Jedwali Na. 2: Tafsiri ya Moja kwa Moja - Majina ya Mahali

| Lugha Chanzi (Kiswahili) | Lugha Lengwa (Kiingereza) | Ukurasa (Matini Tafsiri) |
|---------------------------|---------------------------|--------------------------|
| Kenya | Kenya | uk.6 |
| Tanga | Tanga | uk.6 |
| Tabora | Tabora | uk.23 |
| Machui | Machui | uk. 24 |
| Buguruni | Buguruni | uk.27 |
| Dar es Salaam | Dar es Salaam | uk.27 |
| Nairobi | Nairobi | uk.35 |
| Kampala | Kampala | uk.51 |
| Mwembe Tayari | Mwembe Tayari | uk.54 |
| Dodoma | Dodoma | uk.58 |
| Sumbawanga | Sumbawanga | uk.59 |
| Arabia | Arabia | uk.67 |
| India | India | uk.67 |
| Mtwapa | Mtwapa | uk.67 |
| Tanzania | Tanzania | uk.67 |
| Tononoka | Tononoka | uk.73 |
| Lamu | Lamu | uk.74 |
| Uganda | Uganda | uk.74 |
| Kengeleni | Kengeleni | uk.75 |
| Malindi | Malindi | uk.75 |
| Makadara | Makadara | uk.75 |
| Murang'a | Murang'a | uk.76 |
| Bamburi | Bamburi | uk.78 |
| Lodwar | Lodwar | uk.79 |
| Kisumu | Kisumu | uk.79 |
| Changamwe | Changamwe | uk.82 |
| Makaburini | Makaburini | uk.84 |
| Kibarani | Kibarani | uk.80 |
| Mlaleo | Mlaleo | uk.88 |
| Majengo King'orani | Majengo King'orani | uk.92 |
| Kitale | Kitale | uk.110 |
| Makutano kwa Ngozi | Makutano kwa Ngozi | uk.111 |
| Kisauni Msikitini | Kisauni Msikitini | uk.45 |

Chanzo: Data Kutokana na Uchambuzi wa Riwaya ya *A Good Day*, 2019

Majina ya mahali yalikuwa mengi, hatungeweza kuyaonesha yote. Halikadalika, tulibaini kwamba ukopaji wa moja kwa moja ulitumika katika kutafsiri vipengele vya kiutamaduni kama vile chakula, miti, gari, vinywaji, muziki, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 3 hapa chini.

Jedwali Na. 3: Tafsiri ya Moja kwa Moja - Majina ya Dhana za Kiutamadumi

| Lughaa Chanzi | Lughaa Lengwa | Maana | Ukurasa (Matini Tafsiri) |
|---------------|---------------|-------------------------------|--------------------------|
| Ugali | Ugali | Chakula | uk.69 |
| Mtondoo | Mtondoo | Aina ya mti | uk. 98 |
| Coca Cola | Coca Cola | Aina ya soda | uk.111 |
| Fanta | Fanta | Aina ya soda | uk.65 |
| Matatu | Matatu | Aina ya gari ya abiria | uk. 110 |
| Taarab | Taarab | Aina ya muziki | uk.5 |
| Mwanaharamu | Mwanaharamu | Mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa | uk.9 |
| Msi baba | Msi baba | Asiye na baba | uk.9 |

Chanzo: Data Kutokana na Uchambuzi wa Riwaya ya *A Good Day*, 2019

Wataalamu mbalimbali (Leppihalmed, 1997; Aguilera, 2008; Utami na wenzake, 2018 na Hang, 2018) wamejadili suala la tafsiri ya majina. Kwa mfano, Leppihalme (1997) anapendekeza majina yatafsiriwe kwa njia tatu yaani kuacha jina bila kutafsiri, kubadilisha jina na kudondosha jina. Kulingana na Aguilera (2008), matini hutofautiana na hivyo wafasiri wanaweza kutofutiana katika namna watakavyoamua kutafsiri majina. Hii ni kwa sababu tafsiri hutegemea lengo la mfasiri au la mteja, hadhira lengwa, aina ya matini na muktadha lengwa. Hivyo, mfasiri anaweza kutafsiri majina, mfasiri mwingine akayaacha na mwingine akayadondosha kutegemea vigezo tulivyoelezea. Katika hali hii, inakuwa vigumu kutoa hitimisho la jumla ikiwa majina yanapaswa kutafsiriwa au la. Wafasiri wa *Siku Njema* waliamua kuacha majina yote vile yalivyokuwa bila kuyatafsiri. Kulingana na Vinay na Derbelnet, mkakati wa ukopaji wa moja kwa moja kama huu wa kuhamisha majina vile yalivyokuwa katika LC hutumiwa kwa sababu zifuatazo: kutokuwepo na visawe baina ya LC na LL, kuwepo kwa dhana geni za kiteknolojia, mwandishi kuamua kusawiri ladha ya utamaduni wa lughaa chanzi na kuleta athari ya kimtindo. Waandishi wa makala

Kuna aina ya pili ya ukopaji kuititia mkakati wa utohozi. Kuhusu utohozi, neno mkopo hurekebishwa kuendana na kanuni za kifonolojia na kimofolojia za lughaa lengwa. Jedwali Na. 2 linaonesha mifano ya mkakati wa utohozi.

Jedwali Na. 4: Mifano ya utohozi

| Lughaa Chanzi | Lughaa Lengwa | Ukurasa (Matini Tafsiri) |
|---------------|---------------|--------------------------|
| Televisheni | Television | uk.65 |
| Redio | Radio | uk.5 |
| Hedimasta | Headmaster | uk.20 |
| Paredi | Parade | Uk.20 |

Chanzo: Data Kutoka kwa Riwaya ya *A Good Day*, 2019

ii) Tafsiri Mkopo /Tafsiri ya Dhana (Vinay na Derbelnet, 2004)

Tafsiri ya dhana ni mkakati maalumu wa ukopaji unaohusu tafsiri ya dhana za lugha chanzi na kuingizwa katika lugha lengwa. Mfasiri huchukua hatua anapokosa visawe lingenifu baina ya lugha chanzi na lugha lengwa. Vinay na Darbelnet wanaeleza kwamba neno hukopwa kutoka lugha chanzi na kusilimishwa ili liendane na muundo wa lugha lengwa kwa kubadilisha vipashio vya kifonolojia au/na vya kimofolojia. Pia, vipashio hivi hubadilishwa ili viendane na mpangilio wa kisintaksia wa lugha lengwa. Maneno mengine yaliyoundwa kupitia mkakati huu wa kutafsiri kwa mpito wa wakati hukubalika kama msamiati wa kawaida. Mifano ya maneno ya Kiswahili yaliyoundwa kupitia mkakati huu na hatimaye kukubalika kama msamiati wa kawaida ni kama vile: usiku mwema kutoka kwa *good night*, wako mwaminifu kutoka kwa *yours faithfully*, nachukua nafasi hii kutoka kwa *I take this opportunity* na kadhalika. *Katika riwaya ya siku njema hatukuweza kupata mifano ya mkakati huu isipokuwa mifano mmoja tu.*

Jedwali Na. 5: Mifano ya Tafsiri Mkopo/ Tafsiri ya Dhana

| Lugha Chanzi | Lugha Lengwa | Ukurasa (Matini Tafsiri) |
|--------------|--------------|--------------------------|
| Ugali | <i>Ugali</i> | uk.69 |
| | | |

Chanzo: Data kutoka kwa Riwaya ya *A Good Day*, 2019

iii) Tafsiri Sisisi (Vinay na Derbelnet, 2004)

Tafsiri sisisi ni mkakati wa kuhamisha maana ya lugha chanzi kwenda lugha lengwa kwa kutafsiri neno kwa neno lakini kwa kuzingatia muundo wa lugha lengwa. Kuhusu mkakati huu, Vinay na Derbelnet (2004), wanaeleza kwamba, tafsiri sisisi inahusisha tafsiri ya moja kwa moja ya neno la lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Katika matumizi ya mkakati huu, mfasiri hana nafasi kubwa ya kufuata kanuni za kiisimu za lugha lengwa. Mfasiri hutafsiri maneno kwa kuzingatia maana zake za kimsingi katika lugha chanzi. Kwa mujibu wa Aghajani na Adloo (2018), mkakati huu unafaa katika mchakato wa tafsiri baina ya lugha mbili zinazofanana, yaani lugha nasaba na zinazoshabihiana kiutamaduni.

Jedwali Na. 6: Mifano ya Tafsiri Sisisi

| Lugha Chanzi (Kiswahili) | Lugha Lengwa (Kiingereza) | Ukurasa (Matini Tafsiri) |
|---|--|----------------------------------|
| Siku njema | <i>A good day</i> | Mada/Kichwa cha Kitabu |
| Moyo wangu ni jangwa lisiloweza kuota mapenzi kwa mwanamke. | <i>My heart is a desert where love for a woman cannot grow.</i> | uk.41 |
| Jumuiya ya Afrika Mashariki | <i>East Afrika Community</i> | uk. 51 |
| Nipe nikupe | <i>Give and take</i> | uk.56 |
| Penye nia pana njia. | <i>Where there is a will there is a way.</i> | uk. 60 |
| Mpendaraha | <i>Comfort-lover</i> | uk.68 |
| Mwana wa Mhunzi asiposana huvuvia. | | uk. 69 |
| Swahibu Mahabubu | <i>Beloved Friend</i> | uk. 78 |
| Alitaka awe karibu na kitoto chake, akae nacho, akichuchie, akipakate,akikoshe, akiase, akilishe-muradi akipania kukitunza kama afanyavyo ndege mzazi kwa kinda lake kiotani. | <i>She wanted to be close to her baby, rock him to sleep, hold him, bathe him, guide him, and feed him-like a bird looks after its nestling.</i> | uk.3 |
| Wakipigana na kuchaniana nguo hadharani bila haya | <i>...fought shamelessly in public, tearing each other's clothes to shreds</i> | Uk.1 |
| Mti mkuu ukianguka ndege huwa mashakani. | <i>Woe unto the birds when the giant tree faals.</i> | Uk.2 |
| Rehemwa ilifunga milango yake na kuzitupa funguo kusikofikika kamwe. | <i>Lady luck shut her doors aand threw away the keys.</i> | Uk.10 |
| Unyasi mmoja ukitoka kwenye paa, nyumba haivuji. | <i>The roof does not leak because a blade of grass is missing.</i> | Uk.10 |
| Gangaganga za mganga humlaza mgonjwa na matumaini. | <i>A doctor's continued treatment gives hope to the patient.</i> | Uk.12 |
| Nyimbo zote | Zilitafsiriwa kwa mkakati wa tafsiri sisisi | uk.13, 35, 65-66 |
| Mashairi yote | Mashairi yote yalitafsiriwa sisisi | Uk. 4, 45, 90,101,120 na 140-141 |
| Barua zote | Barua zote zilitafsiriwa kwa kutumia mkakati wa tafsiri sisisi | uk. 34,96-97, 99-100, 125-126 |

Chanzo: Data kutoka kwa Riwaya ya A Good Day, 2019

Kama ilivyokuwa katika mikakati ile mingine, mkakati huu umetumika kwa wingi. Hivyo, hatungeweza kuionesha mifano yote kwa kubanwa na nafasi.

Vinay na Derbelnet wanashauri kwamba ikiwa mfasiri amejaribu kutumia mikakati mitatu ya mwanzo na kutambua kwamba haikubaliki katika muktadha wa kipengele anachotafsiri, basi hatua nyingine ni kutumia mikakati isiyo ya moja kwa moja. Mionganoni mwa mikakati katika mkakati huu ni uhamishaji, ubadilishaji, usawe na tasiri maana.

2. Mkakati Jumla

Mkakati jumla hutumiwa mara nyingi kutafsiri vipashio vikubwa kuliko neno na kirai. Kuhusu mkakati huu wa jumla, Reza (2018) anaeleza kwamba mfasiri anaweza kukabiliana na miundo tofauti ya lugha chanzi na lugha lengwa ambayo haiwezi kuruhusu uhamishaji wa mtindo bila kuvunja sheria za kisintaksia na kileksia za lugha chanzi. Kwa hivyo, mfasiri hulazimika kutumia mikakati ambayo si ya kawaida ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo. Mkakati huu ulibainishwa na Vinay na Derbelnet kuwa mkakati wa jumla au usio wa moja kwa moja ambao una mikakati minne chini yake kama ifuatavyo:

i) Uhamishaji (Vinay na Derbelnet, 2004)

Uhamishaji unahusisha kubadilisha kategoria za maneno kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa bila kubadili maana ya ujumbe. Msingi wa mkakati wa tafsiri wa uhamishaji ni kwamba dhana yoyote inaweza kuelezea kwa njia tofauti bila kuathiri ujumbe uliokusudiwa. Katika mchakato huu, mfasiri anaweza kubadili kitenzi katika lugha chanzi na kuwa kivumishi katika lugha lengwa, nomino kuwa kitenzi, kubadili hadhi ya neno kutoka kiima kwenda yambwa au kutoka neno kwenda kirai, kubadili ngeli ya nomino, kubadili kutoka umoja kwenda wingi na kinyume chake na matumizi ya maneno zaidi ya moja. Halikadhalika, uhamishaji unaweza kutenganisha maneno yaliyounda neno moja na kuwa maneno mawili yanayojitegemea. Wataalamu Vinay na Derbelnet wanatofautisha aina mbili za uhamishaji, uhamishaji wa lazima na uhamishaji wa hiari. Kuhusu matumizi ya mkakati huu, hadhi ya maneno katika LC inaweza kubadilika. Hata hivyo, mfasiri lazima ahakikishe maana haibadiliki. Jedwali Na. 7 linaonesha matumizi ya mkakati wa uhamishaji katika tafsiri ya *A Good Day*.

Data katika Jedwali Na. 7 inaonesha kwamba mkakati wa uhamishaji umetumika hivi kwamba maneno na dhana zimehama kutoka kategoria moja kwenda nyingine. Kwa mfano, neno moja katika lugha chanzi kutafsiriwa na kuwa maneno mawili katika lugha lengwa kama vile: *akipakate* kwenda *hold him*, *akiokoshe* kwenda *bath him*, *akiase* kuwa *guide him* na *kadhalika*. Aidha, kuna kubadilika kwa aina ya maneno ya lugha chanzi kuchukua kategoria nyingine katika lugha lengwa. Kwa mfano, *ukewenza* ni dhana ila inatafsiriwa *co-wife* ambalo ni jina. Pia, neno *redioni* ni kielezi lakini tafsiri yake like *a redio* inakuwa tashbihi.

Jedwali Na. 7: Mifano ya Mkakati wa Uhamishaji

| Lugha Chanzi | Kategoria ya Neno | Lugha Lengwa | Kategoria ya Neno | Ukurasa (Matini Tafsiri) |
|--------------|-------------------|----------------------|---|--------------------------|
| Mpendaraha | Neno moja | <i>Comfort-lover</i> | Maneno mawili yaliyounganishwa na kistari | uk.68 |
| Akipakate | Neno moja | <i>Hold him</i> | Maneno mawili | uk.3 |
| Akikoshe | Neno moja | <i>Bath him</i> | Maneno mawili | uk.3 |
| Akiase | Neno moja | <i>Guide him</i> | Maneno mawili | uk.3 |
| Akilishe | Neno moja | <i>Feed him</i> | Maneno mawili | uk.3 |
| Ukewenza | Dhana | <i>Co-wife</i> | Nomino | uk.1 |
| Redioni | Kielezi | <i>Like a redio</i> | Smile | Uk.5 |

Chanzo: Data Kutokana na Uchambuzi wa Riwaya ya *A Good Day*, 2019

ii) Ubadilishaji (Vinay na Derbelnet, 2004)

Ubadilishaji ni mkakati unaohusisha kubadilishwa kwa mtazamo uliokuwepo katika lugha chanzi ili kukidhi mahitaji ya hadhira lengwa na muundo wa lugha lengwa. Vinay na Derbenet (2004) wanaeleza kwamba mikakati mingineyo haiwezi kutumiwa kuhawilisha ujumbe kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Kwa hivyo, mfasiri hulazimika kuunda mazingira mapya ambayo yanaweza kuwakilisha ujumbe wa lugha chanzi. Hali hii huzua usawe wa kimuktadha na wala si usawe unaojitokeza katika ulinganishaji au usinonimia. Ubadilishaji unahu kubadilishwa kwa muundo wa ujumbe. Mfasiri huwa na uhuru wa kuufinyanga ujumbe wa lugha chanzi na kuuhawilisha kwa njia tofauti huku akidumisha maana iliyokusudiwa. Vinay na Derbelnet wanatofautisha aina mbili za ubadilishaji, ubadilishaji ulio huru na ubadilishaji usio huru (Aghajani na Adloo, 2018). Kwa mfano, mfasiri hana uhuru wa kubadili kipashio cha lugha chanzi kilichokuwa chanya na kukifanya kuwa hasi katika lugha lengwa. Mkakati huu unatumika katika vipashio vikubwa vyta lugha kama vile sentensi, aya au matini nzima. Huu ndio mkakati ambao umetumiwa kutafsiri matini za kidini na vipengele vingine vyta kifasihi (Aghajani na Adloo, 2018). Jedwali Na. 8 linaonesha mifano ya sentensi zilizotafsiriwa kwa kutumia mkakati wa ubadilishaji.

Jedwali Na. 8: Mifano ya Mkakati wa Ubadilishaji (Katika Sentensi)

| Lugha Chanzi | Lugha Lengwa | Ukurasa (Matini Tafsiri) |
|--|--|--------------------------|
| Dau la mnyonge haliendi joshi . | <i>A por man's boat sails slowly.</i> | uK.2 |
| Kama moto katika kichaka kikavu | <i>Like bushfire</i> | uk.3 |
| Si Dar es Salaam si Nairobi si Kampla si Singida si Kigoma si Lamu | Dar es Salaam, Nairobi, Kampala, Singida, Kigoma, Lamu | uk.3 |
| Shoga zake mama | <i>...My mothers female friends</i> | uk.11 |
| Ni kama mtu atakaye kupika ugali akakosa sufuria. | It was like wanting to cook without the cooking pot. | uk.38 |

Chanzo: Data Kutokana na Uchambuzi wa Riwaya ya *A Good Day*, 2019

Vilevile, katika vipashio vikubwa zaidi, wafasiri walitumia mkakati wa ubadilishaji. Kwa mfano, katika uk. 3 katika matini chanzi mwandishi alitumia mtindo wa kishairi na katika hali ya udogo kuelezea mamake Kongowea Mswahili alivyojitelea kumlea mwanawе. Mwandishi anasema:

Alitaka awe karibu na **kitoto** chake, akae nacho, akichuchie, akipakate, akikoshe, akiase, akilishe-muradi akipania kukitunza kama afanyavyo ndege **mzazi** kwa kinda lake kiotani.

Tafsiri ya Kiingereza: *She wanted to be close to her baby, rock him to sleep, hold him, bathe him, guide him, and feed him-like a bird looks after its nestling.*

Matumizi ya uradidi wa ‘aki’ yana dhima ya kishairi na kimsisitizo amba ni mtindo wa mwandishi wa matini chanzi. Hata hivyo, ladha na mvuto huu wa kishairi na kimtindo unapotea katika matini tafsiri. Kutokana na tofauti za kumuundo baina ya Kiswahili na Kiingereza, wafasiri walishindwa kudumisha mtindo huu na kutafsiri tu katika lugha ya kawaida. Hata kama kuna uradidi wa neno ‘him’ mvuto uliokuwepo katika matumizi ya ‘ki’ na kuelezea katika udogo wa mtoto kuwa kitoto uliondolewa kwa kufanyiwa mabadiliko. Ubadilishaji huu ultokana tofauti za lugha chanzi na lugha lengwa.

Aidha, katika uk. wa 46 aya ya pili katika matini tafsiri, ushauri wa Kitwana kwa mpwa wake Kongowea Mswahili unachukua muundo wa kimtindo wa unyambuaji wa maneno ya Kiswahili. Hata hivyo, mtindo huu haungeweza kudumishwa katika matini tafsiri kutokana na tofauti za kumuundo baina ya Kiswahili na Kiingereza. Hivyo, wafasiri walibadilisha mtindo huo na kutumia maneno ya kawaida mradi ujumbe wa kimuktadha umedumishwa kama inavyooneshwa katika mfano ufuatao:

Matini Chanzi: Hurumia wa kuhurumiwa. Msaidie wa kusaidiwa. Ukitumwa tumika.

Matini Tafsiri: *Be kind to the destitute. Help those in need. When you are sent, go.*

Kwa kurejelea tafsiri hii, tunaona kwamba mtindo wa mwandishi asilia wa kuweka muwala na ushikamani wa maneno umepotea. Hata hivyo, ubadilishaji huu haukubadili maana iliyokusudiwa. Ni muhimu kueleza kwamba mkakati wa ubadilishaji unahuishisha kupangua, kudondosha, kuongeza vipengele vya lugha.

iii) Usawe (Vinay na Derbelnet, 2004)

Msingi wa tafsiri ni kuhakikisha maana ya lugha chanzi imehawilishwa kwenda lugha lengwa kwa mwelekeo unaodumisha athari ileile. Hivyo, mfasiri hutumia mkakati wa usawe ili kufanikisha uhamishaji wa maana mbadala. Usawe kwa mujibu wa Vinay na Derbelnet (2004) ni mkakati unaotumiwa na mfasiri ili kuonesha ulinganifu wa ujumbe wa lugha chanzi na lugha lengwa. Ni muhimu kusisitiza kwamba hali hii inaweza kuchangia matini moja kutafsiriwa kwa njia tofauti na wafasiri wawili tofauti. Kiini cha tafsiri inayotumia mkakati wa usawe ni kudumisha ujumbe uleule lakini katika muktadha wa hadhira lengwa na lugha lengwa. Mifano ya matumizi ya mkakati wa usawe ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 9.

Kwa kurejelea data katika Jedwali Na. 9, mkakati wa usawe ulitumiwa kutafsiri maneno: *mama, baba, kaka, shangazi* n.k. Vilevile, mkakati huu ulituimika kutafsiri methali na misemo. Methali na misemo ni vipengele vya kiutamaduni na hakuna lugha moja inayolingana au kufanana katika amali za kiutamaduni. Kwa mujibu wa Venuti (2012), historia ya tafsiri inajengeka katika msingi wa usawe na uamilifu. Anaeleza kwamba fasili ya usawe huelezwa kwa kutumia dhana kama vili '*usahihi*', '*utoshelevu*', '*ulinganifu*' na '*uaminifu*'. Hivyo, lengo kuu la matumizi ya mkakati wa usawe ni kuweza kudumisha athari ileile ya ujumbe wa lugha chanzi kwa hadhira lengwa. Tafsiri za methali na semi ni mifano ya matumizi ya mkakati wa usawe ambapo mfasiri anahitajika kuzingatia usawe au ulinganifu ili kudumisha athari ileile kwa wapokezi wa lugha lengwa.

Kulingana na Nykyri (2010), dhana ya usawe ni dhana pana. Anabainisha aina nne za usawe: usawe kamilifu¹, usawe nusu², usawe kwa upana³ na usawe

¹Tafsiri ya *Complete equivalence*

²Tafsiri ya *partial equivalence*

³Tafsiri ya *broad equivalence*

finyu⁴. Kwa mujibu wa Nykyiri, usawe kamilifu hutokea wakati dhana husika zinapolingana kimaana hivi kwamba zinarejelea kitu kimoja kilichoko katika lugha chanzi na lugha lengwa. Kuhusu usawe nusu, anaeleza kwamba dhana hutofautiana katika lugha chanzi na lugha lengwa. Aidha, dhana inaweza kuwepo katika lugha moja (chanzi) na kutokuwepo katika lugha nyingine (lengwa). Usawe mpana unahu su dhana katika lugha chanzi kuwakilishwa na kundi la dhana au maneno katika lugha lengwa.

Jedwali Na. 9: Mifano ya Mkakati wa Usawe

| Lugha Chanzi | Lugha Lengwa | Ukurasa (Matini Tafsiri) |
|--|--|--------------------------|
| Baba | <i>Father</i> | |
| Mama | <i>Mother</i> | |
| Kaka | <i>Brother</i> | |
| Shangazi | <i>Aunt</i> | |
| Mama Mdogo | <i>Aunt</i> | |
| Babu | <i>Grand Father</i> | |
| Bibi | <i>Grand Mother</i> | |
| Baba Mdogo | <i>Uncle</i> | |
| Baba Mkubwa | <i>Uncle</i> | |
| Mjomba | <i>Uncle</i> | |
| Binamu | <i>Cousin</i> | |
| Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake. | <i>It is the wearer who knows where the shoe pinches.</i> | <i>uk.16</i> |
| ...kungekuwa sawa na kutafuta sindano ndogo katika shamba kubwa la ngano. | <i>...was tantamount to searching for a needle in a haystack.</i> | <i>uk.18</i> |
| Yaliyopita si ndwele tugange yajayo. | <i>It is not good to open old wounds.</i> | <i>uk.33</i> |
| Hatimaye utando uliotandia ufumbuzi wa fumbo la babangu ulianza kutanduka. | <i>At last, the riddle regarding my father began to unravel.</i> | <i>uk.33</i> |
| Kisha akageukajoka la mdimu lichungao watundao. | <i>Latr she became a dog in the manger.</i> | <i>uk.33</i> |
| Mgalla muue na haki yake umpe. | <i>Give credit where it's due.</i> | <i>uk.36</i> |
| Afadhalii kulala katika nyumba ivujayo kuliko kuishi na mwanamke mkorofi. | <i>Better sleep under a leaking roof than live with a difficult woman.</i> | <i>uk.40</i> |
| Msiri kama kaburi | <i>Silent as the grave</i> | <i>uk.44</i> |
| | | |

Chanzo: Data Kutokana na Uchambuzi wa Riwaya ya *A Good Day*, 2019

⁴Tafsiri ya narrow equivalence

Kuhusu usawe unaokaribiana⁵, Panou (2013) naeleza kwamba ni dhana inayotumiwa kuonesha kwamba neno au dhana katika lugha chanzi inaelezwa kwa dhana au neno jingine katika lugha lengwa sawa na hilo lakini lisilolingana. Hii hutokana na tofauti za kiisimu na kiutamaduni ambapo dhana huenda ikakosa kisawe linganifu bainaya lugha chanzi na lugha lengwa. Usawe wa kisemantiki hujitokeza sana katika kamusi. Usawe wa kipragmatiki hudhihirika katika matumizi halisi ya lugha na katika muktadha.

iv) Urekebishaji (Vinay na Derbelnet, 2004)

Urekebishaji ni mkakati unaohusisha kuunda upya ujumbe wa lugha chanzi ili uweze kukubalika katika muktadha wa hadhira lengwa. Mfasiri huchukua uamuzi wa aina hii anapobaini kwamba ujumbe wa lugha chanzi hauwezi kueleweka katika muktadha wa lugha lengwa. Urekebishaji (*adaptation*) kwa mujibu wa Vinay na Derbelnet (2004) ni mkakati unaotumiwa katika muktadha ambapo kinachoeleza katika lugha chanzi hakipo katika muktadha na utamaduni wa lugha lengwa. Hivyo, mkakati huu hutumiwa na mfasiri anapobaini kuwa kuna pengo baina ya lugha chanzi na lugha lengwa. Urekebishaji hutumiwa katika kufasiri mwelekeo wa ujumbe kwa ujumla na wala si vipashio vya lugha. Uchambuzi linganishi baina ya matini chanzi na matini tafsiri unaonesha kwamba wafasiri waliegemea kuwa waaminifu kwa kiasi kikubwa katika kutafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Kuna vipengele vingi vya utamaduni kama methali, semi, tashbihi na sitiari ambavyo badala ya kupewa visawe vyake vilitafsiriwa sisisi. Hivyo, mkakati wa urekebishaji haukuwa na nafasi katika tafsiri ya *Siku Njema* kwenda *A Good Day*.

Kama tulivyoeleza awali, urekebishaji unahuuskuundwa upya kwa ujumbe ili uweze kikitwa katika utamaduni na muktadha wa hadhira lengwa. Katika tafsiri ya *Siku Njema* kwenda *A Good Day*, kuna ugenishaji mwingu ambapo vipengele vya utamaduni wa mswahili au mwaafrika kwa jumla vimehamishwa vile vilivyo na kuingizwa katika lugha ya Kiingereza. Mfasiri alijikita katika kuwasilisha yaliyomo katika *Siku Njema* na wala si kuegemea muktadha wa hadhira lengwa.

Tathmini ya Uteuzi wa Mikakati ya Tafsiri ya *A Good Day*

Waandishi wa makala haya wamebaini kwamba wafasiri walihamisha majina yote ya watu, mahali na vitu kama yalivyokuwa kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa kuititia mkakati wa ukopaji wa moja kwa moja. Kwa kufanya hivyo waliweza kuhamisha utamaduni wa kiafrika hususan wa mswahili na kuuweka

⁵Tafsiri ya *near equivalence*

katika muktadha wa Kiingereza. Kulingana na Mwansoko na wenzake (2015), tafsiri ya aina hii ni nyenzo mojawapo ya kusambaza utamaduni. Hivyo, mkakati wa ukopaji wa moja kwa moja ulitumika kwa kiwango cha juu katika tafsiri ya majina. Vilevile, mkakati wa tafsiri sisisi ulitumika kwa kiwango cha juu katika kutafsiri vipengele vya kiutamaduni hususan methali, misemo, tashbih na sitiari. Tafsiri ya moja kwa moja ya vipengele vya kiutamaduni hupotosha ujumbe. Hii ni kwa sababu hakuna lugha mbili zinazolingana kiutamaduni. Ingefaa kama wafasiri wangejitahidi kupata visawe linganifu vya lugha lengwa ambavyo vingeweza kuakisi muktadha wa lugha lengwa na hadhira lengwa. Vipengele vya kiutamaduni kama vile methali na semi hufungamana na utamaduni na mazingira ya jamii husika hivyo huenda visieleweke katika mazingira ya jamii ya lugha lengwa. Kuhusu tafsiri ya methali na misemo, Toury (2000) anaeleza kwamba katika mchakato wa kutafsiri, vipengele vya kiutamaduni haviwezi kupuuzwa. Anatoa mifano ya vipengele hivi kama vile misemo, methali na sitiari. Kulingana na Rubianti (2019), tafsiri faafu ya semi na methali ni kupata kisawe katika lugha lengwa ambacho kitalingana kimaana na cha lugha chanzi.

Kwa mujibu wa Baker (2007), kuna aina nne za mikakati ya kutafsiri methali na misemo. Mosi, kutafsiri kwa kutumia methali au semi unayolingana kimaana na kimuundo (usawe). Pili, kutafsiri kwa kutumia methali au semi zenye maana sawa lakini zinazotofautiana kimuundo. Tatu, kufafanua maana ya semi au methali. Mkakati huu hutumiwa iwapo hakuna semi na methali zinazolingana baina ya lugha chanzi na lugha lengwa. Nne, kutafsiri kwa kuondoa au kuacha bila kutafsiri. Mfasiri huchukua hatua hii anapokosa kisawe na anapotambua kwamba semi au methali husika haiwezi kufafanuliwa. Vilevile, anaweza kuacha bila kutafsiri kwa sababu zake mwenyewe. Kwa mfano, Kongwea Mswahili akionesha jinsi mambo yalivymwendea mrاما anasema '*Rehema ilifunga milango yake na kuzitupa funguo kusikofikika kamwe*'. Tamathali hii ya semi (sitiari/uhaisaji) imetafsiriwa kwa mkakati wa tafsiri sisisi na kuwa, '**Lady luck shut her doors and threw away the keys**'. Tafsiri hii imepotosha ujumbe uliokusudiwa kwa kuwa neno Rehema halikutumiwa kama jina la mwanamke katika muktadha wa matini chanzi kama ilivyotafsiriwa katika matini lengwa. Mifano ya aina hii ni mingi sana ila hatungeweza kuichanganua yote katika makala haya tumeonesha baadhi katika Jedwali Na. 5.

Aidha, waandishi wa makala haya wamebaini kwamba mkakati wa usawe ulitumiwa kwa kiwango cha juu sana. Kazi kubwa ya mfasiri huwa ni kutafuta visawe baina ya lugha chanzi na lugha lengwa vitakavyofanikisha uhawilishaji wa ujumbe wa mwandishi asilia kwa njia inayofaa. Hivyo, wafasiri walichukua mwelekeo wa kuwa waaminifu katika matini chanzi na kutumia mkakati wa usawe kuhawilisha ujumbe wa lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Pia, mkakati mwingine uliotumiwa ni wa ubadilishaji na uhamishaji ili kukidhi tofauti za kimuundo baina ya Kiswahili na Kiingereza. Mkakati wa utohozi ulitumiwa kwa

kiasi kidogo sana. Katika kitabu kizima tulipata mifano minne tu kama inavyooneshwu katika Jedwali Na. 4. Hii ni kwa sababu utohozi hutokana na dhana ambazo hazipo katika lugha lengwa kama vile za kisayansi na kitekinolojia. Maneno ya aina hii hukopwa na kurekebishwa ili yaendane na muundo wa lugha pokezi (lengwa). Imebainika kwamba Kiswahili hukopa dhana nyingi za kisayansi na kitekinolojia kutoka kwa Kiingereza na si kinyume chake. Hivyo, kwa kuwa tafsiri imefanyika kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza, mkakati wa utohozi haukuwa na nafasi. Mifano minne tuliyotoa ya utohozi ni maneno ya Kiingereza yaliyokopwa na kutoholewa kwenda Kiswahili na wala si ya Kiswahili asilia. Mkakati wa urekebishaji haukutumika, na kama tulivyoeleza awali, wafasiri walitumia mkabala wa kuwa na uaminifu kwa matini chanzi hivyo hawakufanya marekebisho mtazamo wa mwandishi asilia. Halikadhalika, mkakati wa tafsiri dhana au tafsiri mkopo hukutumika. Utafiti uliojenga msingi wa makala haya umebaini kwamba ingawa wataalamu wanatumia istilahi tofauti, wataalamu hawa wanakubaliana kwamba kuna aina kuu mbili za mikakati ya tafsiri, yaani inayotumiwa kutafsiri vipengele vidogo na inayotumiwa kutafsiri matini zima. Hivyo, tunapendekeza kwamba ni muhimu kutumia istilahi ya mikakati ya jumla na mikakati ya moja kwa moja ili kujumuisha mikakati na mbinu pamoja na kuondoa mkanganyiko uliopo kuhusu matumizi ya mbinu za tafsiri na mikakati ya tafsiri. Hali hii tunaifafanua kwa kutumia Kielelezo Na.2 na Kielelezo Na. 3 vinavyofafanua kwamba wataalamu hutumia istilahi tofauti kuelezea mikakati ya tafsiri na mbinu za tafsiri. Vilevile, wanaonesha kukubaliana kwamba kuna mikakati ya aina mbili yaani inayotumiwa kutafsiri vipashio vidogo na inayotumiwa kutafsiri matini nzima.

Kielelezo Na. 2: Mikakati ilio chini ya Mkakati Mahususi



Chanzo: Waandishi, 2019

Kielelezo Na. 3: Mikakati iliyochini ya Mkakati Mkuu wa Jumla



Chanzo: Waandishi, 2019

Hitimisho

Makala haya yamebaini kwamba uteuzi wa mikakati ya tafsiri ina athari chanya na hasi katika uhawilishaji wa ujumbe. Mikakati iliyotumiwa ilifanikiwa kuhawilisha ujumbe wa mwandishi kwenda lugha lengwa kwa njia inayofaa lakini pia ilikuwa na athari hasi kwa kupotosha ujumbe kama ilivyoelezwa hapo awali hususan matumizi ya mkakati wa tafsiri sisisi katika tafsiri ya vipengele vya kiutamaduni. Wafasiri wanapaswa kuwa na weledi wa uteuzi wa mikakati ya tafsiri inayofaa katika kuhawilisha ujumbe kwa njia inayofaa na sadifu. Suala la uteuzi wa mikakati ya tafsiri ni la msingi katika mchakato wa tafsiri ambalo linahitaji kutiliwa maanani na wafasiri, wasomi na watafiti katika uga wa tafsiri.

Marejeo

- Aghajani, M., & Adloo, M. (2018). Procedures Employed in Persian and English Translation of the Last 16 Suras of Quran on the Basis of Vinay and Darbelnet's Model. *Journal of Applied Linguistics and Language Research*, 5(5), 54-66.
- Aguilera, C. E. (2008). "The Translation of Proper Names in Children's Literature." AVANTI Research Group. Chuo Kikuu cha Granada.

- Azar, Z. A. S. (2018). Study of Vinay and Darbelnet's Seven Translation Strategies in Four Translations of Divorce Surah of Quran. *Journal of Teaching English Language Studies*, Vol. 6, 4.
http://tels.tiau.ac.ir/article_540936_01ccf0605caeb4886250df5c11ed55dc.pdf
Iliyorejelewa tarehe 11/6/2019.
- Bell, R. T., & Candlin, C. (1991). *Translation and Translating: Theory and Practice* (Vol. 298). London: Longman.
- Chesterman, A. (1997). *Memes of Translation: The Spread of Ideas in Translation Theory*. Amsterdam: John Benjamins.
- Dai, L. (2015). Translation Strategies for the Chinese Culture-specific Expressions in the Chinese Premier's Press Conferences. *Tasnifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha De Montfort*.
- Dyachkovskaya, V. G. (2018). On Translation Strategies of the Epic Texts. M.K. Ammosov. Chuo Kikuu cha North-Eastern Federal. *Journal of Siberian Federal University. Humanities & Social Sciences*;11 (5), 716-725.
- Hang, T. T. (2018). Translating Proper Names in a Literary Text: A Case of Harry Potter Novel in Vietnam. *VNU Journal of Foreign Studies*, 34(2), 39-50.
- Jilala, H. (2014). "Athari za Kitamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii katika Makumbusho za Tanzania." *Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*.
- Larson, M. (1984). *Meaning-Based Translation*. New York: University Press of America, Inc.
- Leppihalme, R. (1997). *Culture Bumps: An Empirical Approach to the Translation of Allusions, Topics in Translation 10*. Clevedon: Multilingual Matters Ltd.
- Lörscher, W. (1991). *Translation Performance, Translation Process and Translation Strategies: A Psycholinguistics Investigation*. Tübingen: Gunter Narr.
- Malangwa, P. S. (2014). Challenges of Translating Cultural Expressions in Teaching Kiswahili to Foreigners. *Kiswahili*, 77, 104-117. Dar es Salaam: TUKI.
- Malangwa, S. P. (2017). "Mchango, Maendeleo na Changamoto Zinazokabili Taaluma za Tafsiri na Ukalimani." Katika Mosol Kandagor, Nathan Ogechi & Clarisa Vierke (wah.), *Lughā na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja*. Chuo Kikuu cha Moi, 267-277.
- Molina, L., & Albir, H. A. (2002). Translation Techniques Revisited: A Dynamic and Functional Approach. *Meta: Journal des Traducteurs/Meta: Translators' Journal*, 47(4), 498-512.
- Munday, J. (2016). *Introducing Translation Studies: Theories and Application*. London: Routledge.
- Mwansoko, H. J. M., Mekacha, R. D. K., Masoko, D. L. W., & Mtesigwa, P. C. K. (2015). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar-es Salaam: TUKI.

- Newmark, P. (2003). *A TextBook of Translation*. London. Pearson Education Limited.
- Nida, E. A., & Taber C. R. (1969). *The Theory & Practice of Translation*. Chuo Kikuu cha Stanford.
- Nord, C. (1997). *A Functional Typology of Translations*. Amsterdam: John Benjamins.
- Nykyri, S. (2010). *Equivalence and Translation Strategies in Multilingual Thesaurus Construction*. Abo Akademis Förlag: Abo Akademi University Press.
- Ordudari, M. (2007). Translation Procedures, Strategies and Methods. *Translation Journal*, 11(3), 8.
- Pendit, N. P. M. D. (2019). Translation Procedures in the Translation of English Adverbs of Manner(-ly) into Indonesian. *Jurnal Santiaji Pendidikan*, 9(1), 8-13.
- Panou, D. (2013). Theory and Practice in Language Studies. *Theory and Practice in Language Studies*, 3(1), 1-6.
- Pujiastuti, S. (2014). A Survey on Translation Strategies used by Accounting Study Program Students in Translating Undergraduate Thesis Abstracts. Tasnifu ya Stashahada, Chuo Kikuu cha Bengkulu.
- Reza, M. (2018). An Analysis of Translation Procedures in Translated Thesis Abstracts of Students of Faculty of Social and Political Sciences. Tasnifu ya Mtihani wa Sarjana Sastra. Chuo Kikuu cha Sumatera Utara.
- Utami, C. M. D., Puspani, I. A. M., & Sukarini, N. W. (2018). Ideology in Translation of Cultural Lexical Items with Reference to Perburuan and Fugitive. *Litera: Jurnal Litera Bahasa dan Sastra*, 4(1), 60-68.
- Venuti, L. (Ed.). (2012). *The Translation Studies Reader* (3rd Ed.). London: Routledge
- Vinay, J. P., & Darbelnet, J. (1958). *Stylistique Comparée du Francais et de l' Anglais: Méthode de Traduction*. Paris: Didier. Kilichotsiriwa na kuhaririwa na Sager, J.C. na Hamel, M.J. (1995) kuwa *Comparative Stylistics of French and English: A Methodology for Translation*. Amsterdam and Philadelphia: John Benjamins.
- Wafula, M. (2017). Changamoto za Kutafsiri Tamathali za Usemi katika Kufa Kuzikana. Katika Mosol Kandagor, Nathan Ogechi & Clarisa Vierke (wah.), *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja*. Eldoret: Moi University Press, 295-314.

